

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 2322761-5  
Fax No. +255 026 2324218  
E-mail: [info@bunge.go.tz](mailto:info@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 941,  
**DODOMA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MKUTANO WA KUSIKILIZA MAONI YA WADAU JUU YA MUSWADA  
WA FEDHA WA MWAKA 2017**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2016, Nyongeza ya Nane, Sehemu ya Tatu Kifungu cha 9, imepewa jukumu la kusikiliza maoni na mapendekezo ya wadau kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha kila mwaka.

Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ya Bajeti imepanga kufanya Mkutano wa Wadau wote wa masuala ya kodi (**Public Hearing**) kwa ajili ya kusikiliza maoni yao na mapendekezo kuhusu **Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 (Muswada huo unapatikana katika tovuti ya Bunge, [www.Bunge.go.tz](http://www.Bunge.go.tz)).**

Mkutano huo umepangwa kufanyika siku ya Alhamisi na Ijumaa Tarehe **15 na 16 Juni 2017** kuanzia **Saa Tano asubuhi** katika Ukumbi wa Pius Msekwa, Mkoani Dodoma.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Muswada huo, Kamati inawaalika wadau wote kufika na kuwasilisha maoni yao kabla haujapelekwa katika hatua nyingine. Maoni ya wadau yanaweza pia kuwasilishwa kwa njia ya Posta au Barua pepe kwa anuani ifuatayo:

Katibu wa Bunge,  
Ofisi ya Bunge,  
S.L.P 941,  
**DODOMA**  
Barua pepe: [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)

**Imetolewa na,**

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano.  
Ofisi ya Bunge,  
S.L.P 941,  
**DODOMA**

12 Juni, 2017.